# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA SABA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA MOJA

**12 MEI, 2022**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA SABA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA MOJA – TAREHE 12 MEI, 2022

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA MAJI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:**

## IV. MASWALI YA KAWAIDA:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**182. MHESHIMIWA ZACHARIA PAULO ISSAAY (MBULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaajiri Watumishi 40,000 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ilivyopitishwa katika Bajeti ya 2021/2022.

**183. MHESHIMIWA IDDI KASSIM IDDI (MSALALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali inaichukulia hatua gani TARURA Msalala kwa kuchelewesha Mikataba na kuwapa kazi Wakandarasi wasio na uwezo.

**WIZARA YA AFYA:**

**184. MHESHIMIWA LUCY JOHN SABU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza vifo vya Akinamama Wajawazito.

**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:**

**185. MHESHIMIWA TARIMBA GULAM ABBAS (KINONDONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, nini juhudi za Serikali kuweka mifumo rafiki ya kurahisisha ufanyaji wa biashara ili kuvutia zaidi uwekezaji nchini.

## WIZARA YA NISHATI:

**186. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON MWAKAGENDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itaongeza fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa REA III katika Wilaya za Busokelo na Rungwe.

## WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**187. MHESHIMIWA ANNA RICHARD LUPEMBE (NSIMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Daraja la Ugalla lililopo katika Kata ya Ugalla.

## V. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI WA MAJI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**DODOMA**
**12 MEI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**KATIBU WA BUNGE**